MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA
(DUWASA)

SIMU: 026 - 2324245 Tovuti: www.duwasa.go.tz S.L.P. 431
FAKSI: 026 - 2320060 Imeli:md@duwasa.go.tz DODOMA

MATUMIZI MAZURI YA MTANDAO WA MAJITAKA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) inawakumbusha wateja wake na wananchi wote kwa ujumla kutumia vyema mfumo wa mtandao wa majitaka ili kuepusha mtandao huo kuziba mara kwa mara. Aidha ikumbukwe kuwa mtandao wa majitaka ni kwa ajili ya taka laini na hairuhusiwi kutupa taka ngumu kwenye mfumo wa majitaka.

Tahadhari hii inawahusu wananchi wote ambao wameungwa kwenye mfumo wa mtandao wa majitaka na wale ambao hawajaungwa kwenye mfumo wa majitaka pia. Inapotokea taka ngumu zikatupwa kwenye mfumo wa mabomba ya majitaka inasababisha kuziba kwa mfumo wa majitaka na kusababisha kero kwa wananchi wengine pamoja na kuweza kusababisha hatari ya magonjwa kutokana na uchafu ambao unakuwa umeziba na kutapakaa mitaani.

Hivyo, wananchi wote tunahimizwa kujenga chekeche juu ya chemba za majitaka kwa lengo la kuzuia taka ngumu kuingia kwenye mfumo wa majitaka.

“Maji ni Uhai na Usafi wa Mazingira ni Utu”

Tangazo hili limetolewa na:

Eng. David T. Pallangyo
MKURUGENZI MTENDAJI
DUWASA
18/08/2018

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA
(DUWASA)

SIMU: 026 - 2324245 Tovuti: www.duwasa.go.tz S.L.P. 431
FAKSI: 026 - 2320060 Imeli:md@duwasa.go.tz DODOMA

TANGAZO

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) inawakumbusha wateja wake na wananchi wote kwa ujumla ikiwa ni pamoja na wa maeneo ya majumbani, maofisini na sehemu zote za biashara na huduma kuwa na vihifadhio vya maji. Vihifadhio hivyo vinaweza kuwa ni matenki ya maji ambayo huwa ni yenye ujazo mbalimbali kulingana na idadi ya watu wanaoishi katika eneo husika au hata majaba iwapo eneo hilo ni la watu wachache.

Utamaduni wa kuwa na vihifadhio vya maji ni mzuri na unawahakikishia wananchi uhakika wa kuwa na huduma ya maji wakati wote hata iwapo panatokea katizo la huduma kwa sababu mbalimbali.

Tangazo hili limetolewa na:

Eng. David T. Pallangyo
MKURUGENZI MTENDAJI
DUWASA
18/08/2018

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA
(DUWASA)

SIMU: 026 - 2324245 Tovuti: www.duwasa.go.tz S.L.P. 431
FAKSI: 026 - 2320060 Imeli:md@duwasa.go.tz DODOMA

TANGAZO

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) ipo katika hatua za mwisho za utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa mitandao ya mobomba ya majisafi katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma. Lengo la ujenzi huo wa miradi ni kuwafikia wananchi ambao walikuwa mbali na mitandao ya mabomba ya majisafi pamoja na kuongeza vipenyo vya mabomba ili kukidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wa maeneo husika. Maeneo ambayo yamehusika na ujenzi wa miradi hii ni pamoja na: Veyula Kambarage, Veyula Muungano, Ndachi Mtube, Ndachi *West*, Nzuguni A, B na C, Ilazo *Extension*, Mapinduzi/Makulu, Iyumbu, Nhyuka, Chinangali *North*, Chinangali *West*, Mbwanga, na Image.

Hivyo, wakazi wa maeneo husika wanahimizwa kufika ofisi kuu DUWASA ili taratibu za kuwaunganisha kwenye mfumo wa maji ziweze kufanyika. Kila mwananchi ahakikishe kuwa anafika DUWASA na kuonana watumishi husika ambao wanafanya kazi za maunganisho ya maji na wasikubali kutapeliwa na Vishoka.

Ndugu Mwananchi, furahia huduma ya maji kwa kuwa na maunganisho ya maji nyumbani kwako – DUWASA ina maji ya kutosha kukuhudumia wewe.

Tangazo hili limetolewa na:

Eng. David T. Pallangyo
MKURUGENZI MTENDAJI
DUWASA
18/08/2018

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA
(DUWASA)

SIMU: 026 - 2324245 Tovuti: www.duwasa.go.tz S.L.P. 431
FAKSI: 026 - 2320060 Imeli:md@duwasa.go.tz DODOMA

TANGAZO LA DUWASA

Ndugu mteja, DUWASA inaendesha zoezi la uhakiki wa namba za simu za wateja wake wote kwa lengo la kuhakikisha kuwa namba hizo za simu ni sahihi na ni za walengwa ambao wanatakiwa kutumiwa bili za maji za kila mwezi. Ni muhimu namba ya simu ambayo ni sahihi ya mteja ikawepo DUWASA ili mteja aweze kupata taarifa mbalimbali za Mamlaka kama vile bili za maji za kila mwezi, taarifa za kukatika kwa huduma ya maji pale inapotokea na taarifa zozote ambazo ni muhimu kujulikana na mteja.

Ikumbukwe kuwa wateja wote wa DUWASA wanatumiwa bili zao za maji kwa njia ya simu zao za mikononi hivyo ni muhimu sana kuhakikisha namba yako ipo DUWASA. Hivyo basi, namba yako kama haipo DUWASA na huwa hupati taarifa za DUWASA, mpatie namba yako ya simu Mtumishi aliyekupatia tangazo hili au tuma namba yako ikiwa na majina, akaunti yako ya uteja wa maji au namba ya mita ya maji kwa **namba 0767000207 au 0767000208** au fika ofisi kuu za **DUWASA**. Zoezi hili ni muhimu sana na tunaomba sana ushirikiano wa kila mteja.

Aidha ikiwa mteja hupati bili yako ya maji ya kila mwezi unaweza kuipata pia kwa kutumia simu yako ya mkononi kwa kupiga *152*00# unachagua namba 6 ambayo ni maji halafu unachagua namba 1 ambayo ni DUWASA kisha unachagua namba 1 malipo ya maji na utatakiwa kuingiza namba ya akaunti ya uteja ambayo kila mteja ana akaunti namba yake. Baada ya hapo utapata deni unalodaiwa pamoja na namba ya kumbukumbu ya malipo. Namba hiyo ya malipo hubadilika kila mwezi.

Tangazo hili limetolewa na:

Eng. David T. Pallangyo
MKURUGENZI MTENDAJI
DUWASA
18/08/2018